

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS - TAMISEMI**



Namba za simu

Mkuu wa shule :- 0622 255 320 / 0765 346 576

Makamu Mkuu wa Shule:-0766 335 555

Shule ya Sekondari Binza

S.L.P 319

Tarehe:- 14/12/2020

---

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi.....

.....

S.L.P .....

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI BINZA,  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA MKOA WA SIMIYU MWAKA 2021.**

1. Hii ni kukutaarifu kuwa mwanao aliyetajwa hapo juu amechaguliwa kujiunga na Shule hii kwa mwaka 2021. Hii ni baada ya kuhitimu vizuri elimu ya msingi na kufaulu mtihani wa Taifa Darasa la Saba mwaka 2020.

**2. UTANGULIZI:**

Ni matumaini yangu kuwa mwanao ataitumia vizuri nafasi hii adimu, kusoma kwa bidii, nidhamu na maarifa ili kudhihirisha kuwa haikuwa makosa kwake yeye kuchaguliwa.

**3. KUFUNGUA SHULE:**

Shule itafunguliwa kwa wote siku ya Jumatatu 11, Januari, 2021 asubuhi. Siku hiyo, ufike Shuleni na mwanao ukiwa na mahitaji yote muhimu ya Shule.

**4:0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**4:1) SARE YA SHULE.**

**a) Kwa Wasichana .**

- i) Sketi mbili (2) za rangi ya ugoro (dark brown) zenye malinda (pleats/frills) ya wastani ya kuelekea upande mmoja . Urefu wa sketi uwe ni wa kupita magoti na kugusa visigino. Mkanda wake (waist band) usizidi nchi mbili .
- ii) Blauzi/shati nyeupe mbili za kitambaa cha tetron . Zisiwe za kubana mwili na ziwe za mikono mifupi.
- iii) Viatu ni jozi mbili, viwe ni vya rangi nyeusi tu vya kamba na visiwe na urembo. vifunike miguu na viwe vya visigino vifupi.
- iv) Soksi ziwe nyeupe tu, ndefu kufikia magoti au fupi za kawaida.
- v) T/Shirt rangi nyekundu yenye nembo na maandishi ya Shule.
- vi) Sweta za rangi ya ugoro zisizo na mapambo wala michoro.
- vi) Viatu (raba zenye kamba) kwa ajili ya michezo na shughuli za nje tu.
- vii) Vazi la Hijjab (kwa Waislamu), kitambaa cha shule, kikiwa rangi ya ugoro chini na tetroni nyeupe juu.

## **b) Kwa Wavulana**

- i) Suruali mbili za rangi ya ugoro (dark brown) zenye marinda mawili, mifuko isiyo ya kubandika na za kuvalia kwa mkanda lakini zisizobana . Pia upana wa chini mguuni uwe inchi 16. Jeans/Dengrees haziruhusiwi.
- ii) Shati mbili nyeupe za tetron mikono mifupi . Kila mara Shati daima itachomekwa ndani ya suruali ivaliwapo.
- iii) Viatu ni jozi mbili .Viwe ni vya rangi nyeusi tu vya kamba na visiwe na urembo. Pia viweze kufunika miguu na viwe vya visigino vifupi .
- iv) Soksi ziwe ni nyeupe na hasa ndefu .
- v) T/Shirt rangi nyekundu yenye nembo na maandishi ya Shule.
- vi) Sweta za rangi ya ugoro zisizo na mapambo wala michoro yoyote.
- vii) Viatu vya raba vyeusi kwa ajili ya michezo na shughuli za nje tu .
- viii) Mkanda mweusi wa kiuno (upana inchi 1.5) kufungia Suruali .

## **c) Unadhifu wa Wanafunzi**

-Mwanafunzi sharti aonekane nadhifu wakati wote .

-Heshima kwa viongozi wa serikali, walimu,wafanyakazi wengine,wanafunzi wenzake na jamii kwa ujumla.

-Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote pamoja na kutunza mali za umma.

-Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa pamoja na kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.

-Kufahamu mipaka ya shule.

-Wanafunzi wote watatunza nywele zao zikiwa fupi . Ni marufuku kwa mwanafunzi kufuga nywele ndefu ama kuweka dawa (curl au relaxer).

-Mwanafunzi haruhusiwi kunyoa kipara, panki, na kunyoa nyusi za macho/usoni.

-Mwanafunzi haruhusiwi kupaka kucha rangi na au kutunza kucha ndefu

### **4:2) MAHITAJI YA SHULE:**

Mwanafunzi atatakiwa kufika shuleni na mahitaji yafuatayo:

- Madaftari makubwa 12 kulingana na idadi ya masomo.
- Vifaa kama rula, kalamu n.k
- Mfagio wa kienyeji, mkubwa na uliofungwa vizuri.

### **4:3). SHERIA ZA SHULE:**

- Shule hutoa malezi na kusimamia maadili ya wanafunzi kwa kupitia walimu na walezi wengine. Hivyo ni wajibu wa kila mwanafunzi awapo ndani au nje ya Shule kuonyesha utii , heshima na nidhamu kwa walimu wake na wafanyakazi wasio walimu .


- Ni wajibu wa kila mwanafunzi pia kutii na kutekeleza maagizo na maelekezo apewayo na walimu na walezi wake .
- Wakati wa kuripoti Shuleni , mwanafunzi atapewa nakala ya Sheria za Shule na atatakiwa azisome kwa makini na kuziishi .Hata hivyo ,naweka hapa chini bayana makosa yatakayosababisha mwanao kufutwa ama kufukuzwa Shule endapo atabainika kuyatenda .

- i) Wizi
- ii) Uasherati,ubakaji,ushoga na ulawiti .
- iii) Ulevi wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya .
- iv) Makosa ya jinai
- v) Kupigana au kumpiga mwanafunzi mwenzake, mwalimu au mlezi wake.
- vi) Kuo au kuolewa.
- vii) Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya Shule.
- viii) Kugoma ,kuchochea migomo na au kukataa adhabu iliyotolewa na mwalimu
- ix) Utoro wa muda mrefu hadi kufikia siku tisini mfululizo .
- x) Kumiliki vitu vilivyokatazwa kama simu za mkononi, radio, bangili, kofia, heleni na mikufu .
- xi) Kukataa kufanya mitihani au mazoezi ya masomo .
- xii) Uvaaji mbaya wa sare za Shule kama vile mitindo ya “KK na mayenu”.
- xiii) Kudharau bendera ya Taifa na au nyaraka za Taifa.
- xiv) Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi .

NB: Soma kwa makini maagizo/maelekezo yaliyoko kwenye fomu hii uyazingatie na kuyatekeleza kwa vitendo.

KARIBU SHULE YA SEKONDARI BINZA - KITOVU CHA TAALUMA.

Ahsante,




---

AMEDE M. NDONJE  
MKUU WA SHULE

HEAD MASTER  
BINZA SEC. SCHOOL  
MASWA.

**SEHEMU B**

Sehemu hii ijazwe kwa ushirikiano na mzazi/mlezi

**5. MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI/MZAZI.**

- i) Jina kamili la mwanafunzi.....
- ii) Tarehe ya kuzaliwa.....mwezi.....mwaka.....
- iii) Uraia.....kabila.....
- iv) Dini yake .....dhehebu la .....
- v) a)Jina la Baba ..... hai/siyo hai.  
b)Jina la mlezi.....  
c)Kazi ya baba /mlezi.....  
d) Baba /Mlezi anaishi .....kata .....
- e)Anuani ya Baba /Mlezi .....
- f)Namba ya simu ya mkononi ya baba/mlezi.....
- vi) Taja tatizo la kiafya/maumbile alilonalo (onyesha cheti kama kipo ).....  
.....

**6. TAMKO LA MZAZI /MLEZI.**

Mimi .....Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi huyu, nakubali mtoto wangu asajiliwe katika Shule ya kutwa ya Binza Sekondari .

Ninaahidi kutoa ushirikiano wa karibu katika kumlea na kumwendeleza kitaaluma. Aidha nakubali kumwezesha kikamilifu kwa kumpatia mahitaji yake muhimu ya .....shule ili aweze kutulia Shuleni na kuweka bidii katika masomo yake.

Jina.....Sahihi.....Tarehe.....

**MASWA DISTRICT COUNCIL**

**MEDICAL EXAMINATION REQUEST FORM.**

To be filled by an Authorised Government Medical Officer and returned to School.

**From:** Binza Secondary School,  
P.O.BOX 319,  
MASWA.

**To:** THE MEDICAL OFFICER,  
.....  
.....

**Ref:** .....(a student ).

Please examine the above named student to ascertain his/her physical and mental fitness for a fulltime schooling course at this school .The examination should include categories I-IV.

- I: a) Eye sight:..... h) Asthma:.....
- b) Hearing:..... i) Heart problem:.....
- c) Limbs:..... j) Kidney:.....
- d) Speech:..... k) Peptic ulcers:.....
- e) Venereal diseases:..... l) Epilepsy:.....
- f) Sickle cell anaemia:..... m) Leprosy:.....
- g) Tuberculosis (TB):.....

II: Neurosis.....

III: Other serious Diseases.....

IV: Pregnancy .....

I (Full name).....have examined the above named and consider that he /she is Physically **fit /unfit** for a full time schooling course .

**Designation**.....**Signature**.....

**Date**.....**Rubber stamp**.....